# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**MOI GIRLS ELDORET**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

# MOI GIRLS ELDORET KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**Karatasi ya 1**

**INSHA**

**MWONGOZO**

1. Kumekuwa na ongezeko la migomo ya wafanyakazi nchini katika siku za hivi karibuni. Wewe ni katibu wa tume iliyobuniwa na rais kuzamia suala hili. Andika ripoti

   Muundo.
   - Hii ni insha ya ripoti rasmi.
     Kichwa
   - Anwani andikwe kwa herufi kubwa na iwe kamilifu.
   - Anwani ibaini kiini cha ripoti(suala kuu linalochunguzwa)
   - Bainisha kipindi cha ripoti

2. Utangulizi
   - Mteuzi
   - Haja au sababu
   - weka wazi muda ambao uchunguzi ulifaa kuchukuwa
   - Wahusika (majina ya wanachama yaorodheshwe kuanzia kwa jina la mwenyekiti).

   **Mbinu za kukusanya data**
   - Kuzuru
   - Kuhoji
   - Hojaji.

3. **Matokeo**
   -mishahara midogo
   -mazingira magumu ya kikazi
   - ukosefu wa vifaa muhimu vya kazi
   -mapendeleo kazini
   -uwepo wa sheria/kanuni kandamizi
   -Ukosefu wa kandarasi
   -Dhuluma za mapenzi
   -Ufisadi
   - kufutwa /kucheketwa kwa wafanyakazi
   - kucheleweshwa kwa marupurupu ya uzeeni

4. **MAPENDEKEZO**
   -Pana haja ya kubuni utaratibu wa kuimarisha mishahara ya wafanyakazi
   -Washika dau kuhakikisha kuwa mazingira ya kazi ni wezeshi
   - Kuwepo kwa vifaa muhimu vya kazi
   -Kuwe na hali ambapo wafanyakazi wote wanachukuliwa sawa kazini
   -Maadili ya kikazi kuzingatiwa
   -Kubuniwa kwa sheria zisizovunja motisha ya wafanyakazi
   -Kila mfanyakazi kupewa kandarasi kama njia ya kuonyesha uthabiti wa kazi
   -Wafanyakazi wanaostaafu kupewa marupurupu yao kwa wakati ufaao
   -Waajiri kukoma kuwafuta/kuwacheketa wafanyakazi kiholela

**5.0 Hitimisho**

-Ripoti ihitimishwe kwa kufanya rejea ya matokeo ya utafiti

-Jopo lionyeshe namna ambavyo utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa taifa kwa jumla hasa katika mchakato wa kupunguza au na kuondoa kabisa migomo ya wafanyakazi nchini.
-Tume idhihirishe wazi kuwa kubuniwa kwake kulikuja kwa wakati unaofaa
-Katibu aonyeshe ni vipi ambavyo utafiti huu utasaidia katika kuzuia migomo katika siku za halafu
**Kitambulisho** – Ripoti imeandaliwa na;
-Sahihi
-Jina
-Cheo
-Tarehe .

**Tanbihi.**

1. Asipozingatia muundo wa ripoti aondolewe alama 4 za sura.
   Lazima awe na vipengele vinne au zaidi.
2. Hoja zisipungue tano la sivyo atakuwa amepungukiwa kimaudhui.
3. Mtahiniwa atimize urefu wa insha.**(Maneno 400)** Viwango mbalimbali vya urefu vizingatiwe katika kumkadiria mtahiniwa.
4. Jina la mwanafunzi lijitokeze kama katibu la sivyo atakuwa amepungukiwa kimtindo.
5. Atakayeandika ripoti ya kawaida na awe amezungumzia vipengele hivi atakuwa amepotoka – **Atuzwe D 03/ 20.**6. Atakayekosa kujihusisha katika uandishi wa ripoti atakuwa amejitungia swali. **Atuzwe D – 02/20**

2. **Ufisadi umechangia pakubwa kuwepo kwa maendeleo duni nchini. Jadili**Hili ni swali la kujadili. Mtahiniwa anahitajika ashughulikie pande zote mbili za mada.

- Mtahiniwa aweza kukubaliana na mada kuwa kwa kiwango kikubwa maendeleo duni yamechangiwa na ufisadi na kuwepo kwa ufisadi au aonyeshe kuwa si kwa kiwango kikubwa vile kwani kuna sababu nyingine zinazochngia maendeleo duni nchini.
- Kwa vyovyote vile, pande zote za mada zishughulikiwe. Haijailishi kama upande mmoja utakuwa na hoja nyingi kuliko upande mwingine.

Baadhi ya hoja ni:
**Kuunga mkono**

- Kwa sababu ya hongo, kiasi fulani cha pesa za miradi hutolewa kama hongo. Hali hupunguza kiasi cha pesa za kuteleleza mradi husika.
- Kwa sababu ya ufisadi, utekelezaji wa miradi huwa wa kiwango cha chini.
- Wanaofaa kuhakikisha kuwa kuna viwango vya juu vya utekelezaji wa miradi huhongwa na hivyo kuidhinisha kazi duni.
- Kandarasi za miradi ya maendeleo hutolewa kwa wanakandarasi fisadi ambao pengine hawana ujuzi katika kufanikinisha mradi husika au ambao watatumia vifaa duni ili faida yao iwe kubwa.
- Wafadhili hukataa kuipa nchi pesa za kufadhili miradi fulani kwa hofu ya pesa hizo kutumika vibaya, hivyo basi miradi mingi haipati pesa za kutosha.
- Kuna ubadhirifu wa pesa za miradi na wanaosimamia hazina za maendeleo hivyo kuinyima miradi ya maendeleo pesa zinazohitajika.

**Kupinga**

- Hakuna pesa za kutosha nchini za kufadhili miradi mingi ya maendeleo.
- Utekelezaji mbaya wa miradi waweza kutokana na ukosefu wa vifaa bora nchini kwa hivyo vinavyotumiwa vikawa na matokeo duni.
- Kwa sababu ya siasa, miradi ya maendeleo ikatelezwa visivyo hasa katika sehemu ambayo ni ngome ya mpinzani.

- Wakati mwingine pesa za kutekeleza miradi hutumika kununulia vitu kama magari, kulipa mishahara, kulipa marupurupu nk badala ya kugharamia miradi.

**TANBIHI**
**Zingatia hoja zozote nyingine mwafaka.**

3. Baniani mbaya kiatu chake dawa.

Maana.kiatu cha baniani ni kitu au kundi la watu limechukia au kudharau
Dawa: Kitu husika huendakikawa ndicho jibu au jawabu au suluhisho kwa tatizo fulani maishaninmwa mtu au katika jamii

Mtahiniwa aandike kisa kuthibitishabmatumizi haya ya methali
Mtahiniwa nyingine zenye maana sawa ni;

- Matango na matikiti ndio maponya nja
- Wembamba wa reli gari moshi hupita
- Nyumba nzuri si mlango fungua uingie

Utuzaji

(i) Pande zote za methali zishughulikiwe.Anayeshughulikia upande moja asipite alama C 08/20
Anayetaja tu upande wa pili bila maelezo kikamilifu achukuliwe kuwa amelenga lakini ana udhaifu wa maudhui

(ii) Anayekosa kulenga katika kisa chake amepotoka kimaudhui alama D 03/20

**Swali la nne**

Mtahiniwa ahitimishe insha yake kwa maneno aliyopewa
Kisa chake kifungamane na mawazo ya kauli aliyopewa
Kisa kilenga tukio lilizua taharuki miongoni mwa wahusika
Tukio lenyewe lazima lidhiirishe maafa /maangamizi
Lazima litokee kwenye sehemu iliyozingirwa kama vile ndani ya nyumba,katika gari n.k
Mtahiniwa atumie nafsi ya tatu hali ya wingi(warejelewa)
Atumie wakati uliopita.